REF. PSLE 2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# RATIBA YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI
# (PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION TIMETABLE)
# SEPTEMBA, 2021

| TAREHE NA SIKU | MUDA (SAA) | NAMBA MFICHO | SOMO |
|---|---|---|---|
| **08.09.2021**<br>**JUMATANO** | 2:00 – 3:40 | 01 | KISWAHILI |
| | **3:40 – 4:30** | | **MAPUMZIKO** |
| | 4:30 – 6:30 | 04<br>04E | HISABATI<br>MATHEMATICS |
| | **6:30 – 8:30** | | **MAPUMZIKO** |
| | 8:30 – 10:00 | 03<br>03E | MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI<br>SOCIAL STUDIES AND VOCATIONAL SKILLS |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **09.09.2021 ALHAMISI** | 2:00 – 3:40 | 02 | ENGLISH LANGUAGE |
| | **3:40 – 4:30** | | **MAPUMZIKO** |
| | 4:30 – 6:00 | 05<br>05E | SAYANSI NA TEKNOLOJIA<br>SCIENCE AND TECHNOLOGY |
| | **6:00 – 8:00** | | **MAPUMZIKO** |
| | 8:00 – 9:30 | 06<br>06E | URAIA NA MAADILI<br>CIVIC AND MORAL EDUCATION |

**MAELEKEZO MUHIMU**

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Mtihani ya mwaka 2021** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenye maswali ya mtihani, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Mtihani**.

3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo ndani ya Karatasi ya Mtihani** na **Ratiba ya Mtihani**, **maelekezo yaliyomo katika karatasi ya Mtihani husika ndiyo yatakayofuatwa**.

4. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa Mtihani wa **Kiswahili, 'English Language', Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na Uraia na Maadili.**

5. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa mtihani wa **Hisabati**.

6. Msimamizi wa watahiniwa **WASIOONA** awe Mtaalamu mwaminifu aliye na **uwezo wa kusoma maandishi na alama za 'Braille'**.

7. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za mtihani na za kujibia zenye **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.

8. Karatasi zenye majibu ya watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** zifungwe kwenye **bahasha za pekee**. Zisichanganywe na karatasi za watahiniwa wenye Uoni wa kawaida.

9. Watahiniwa waelekezwe;
   (a) Kuingia ndani ya chumba cha Mtihani nusu saa kabla ya muda wa Mtihani na watakaochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya Mtihani kuanza hawataruhusiwa.
   (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa Mtihani.
   (c) Kuandika namba ya Mtihani kwa usahihi.
   (d) Kuhakikisha namba iliyoandikwa kwenye msimbomilia na namba ya Mtihani zinafanana.
   (e) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina ya watahiniwa. Ikiwa mtahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa Mtihani.
   (f) Watakaojihusisha au watakaofanya udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya Mtihani.